Northern Territory Government

DEPARTMENT OF **HEALTH**

Centre for Disease Control

Mantoux test

*Kipimo cha Mantoux*

Swahili

March 2012

Machi 2012

# The Mantoux Test

# Kipimo cha Mantoux

***(tuberculin skin test)***
***(kipimo cha tuberculin kupitia ngozi)***

## Why do a skin test?

## Kwa nini kufanya kipimo cha ngozi?

Wakati mwingine watu wanaweza kuambukizwa na vijidudu vya kifua kikuu (TB) bila kupata ugonjwa halisi. Kipimo cha Mantoux (kipimo cha tuberculin kupitia ngozi) kinaweza kuonyesha kama mtu aliwahi kuambukizwa na vijidudu vya TB. Maambukizi ya TB hayamanishi kwamba mtu ana ugonjwa, lakini kama mtu ameambukizwa kuna uwezekano wa kupata ugonjwa wa TB katika siku zijazo.

## Who needs a skin test?

## Nani ambaye anahitaji kipimo cha ngozi?

- Mtu fulani ambaye hivi karibuni alikuwa na mawasiliano na mtu ambaye ana ugonjwa wa TB. Watu hao wanaweza kuwa wanafamilia, marafiki, au wafanyakazi wafanyao kazi pamoja..
- Wale ambao wana eksirei inayopendekeza kuwa waliwahi kuwa na ugonjwa wa TB ambao haukutibiwa katika siku za nyuma.
- Watu ambao wana kingamaradhi ya hali ya chini kama vile maambukizo ya VVU (Virusi Vya Ukimwi) au baadhi ya hali ya kitabibu.
- Watu ambao wanatakiwa kupimwa kwa sababu za ajira au kama sehemu ya mpango wa uchunguzi wa shule (kwa sharti kwamba hawakuwa na kipimo cha Mantoux cha hakika hapo awali).
- Kabla ya kutoa BCG kwa watoto wachanga wenye umri wa zaidi miezi 6.
- Watu wanaokaribia kupewa sehemu ya mwili au organ donation kwa lugha ya kigeni.
- Watu wanaosafiri kuenda kwenye nchi hatari.

## The Mantoux test

## Kipimo cha Mantoux

Kipimo cha Mantoux ni kipimo rahisi na salama . Kiasi kidogo cha tuberculin chenye kusafishwa kitokanacho protini ( Tubersol®) kinaingizwa chini tu ya safu ya juu ya ngozi kwenye mkono wa mtu kutumia sindano ndogo safi kabisa na sirinji. Mjibizo wa ngozi (uvimbe) unapimwa siku 2 hadi siku 3 baadaye na matokeo yanawekwa kwenye kumbukumbu.



## Possible side effects

## Athari ambazo zinawezekana

Athari siyo kawaida. Hata hivyo, mtu ambaye amekuwa karibu na vijidudu vya TB anaweza mara kwa mara kuwa na mjibizo kubwa kiasi, ambao unaweza kusababisha baadhi ya usumbufu. Uvimbe huu lazima utatoweka katika muda wa wiki 2.

Mjibizo unaweza kuwasha. Ni bora kutojikuna mkono – kigandamizo cha baridi kinaweza kusaidia kupunguza kuwashwa kokote.

## What does a negative result mean?

## Matokeo hasi anamaananisha nini?

Kama uvimbe ni chini ya ukubwa fulani matokeo ya kipimo ni hasi. Kawaida hii ina maana kwamba mtu hajawahi kuambukizwa na vijidudu vya TB. Hata hivyo, chini ya baadhi ya mazingira inaweza kuwa hasi hata kama mtu ameisha ambukizwa. Hii inaweza kutokea kama mtu amekuwa karibu na TB katika wiki chache zilizopita na mwili haukuwa na muda wa kuendeleza mjibizo au kama ulinzi wa mwili ni dhaifu na hauwezi kuonyesha hisia kwa kipimo cha ngozi. Katika hali hii kipimo kinaweza kurudiwa au kufasiriwa tofauti.

## What does a positive test mean?

## Kipimo hakika inamaanisha nini?

Ina maana kwamba mtu ameathirika na vijidudu vya TB, lakini haimanishe kwamba yeye ana ugonjwa wa TB . Mtu huyu hawezi kuambukiza TB kwa mtu mwingine yeyote isipokuwa inaweza ikaendelea katika tarehe ya baadaye kwenye ugonjwa hai wa TB .

## How can a person be infected and not have TB disease?

## Jinsi gani mtu anaweza kuambukizwa na asikuwe na ugonjwa wa TB?


Baada ya vijidudu vyaTB kuingia mwili, mara nyingi, ulinzi wa mwili unadhibiti vijidudu kwa kujenga ukuta unaovizunguka , kama vile kigaga kinavyojiunda kwenye kidonda. Vidudu vinaweza kuendelea kuishi ndani ya kuta hizi kwa miaka katika hali ya 'utulivu' au uficho. Wakati

vijidudu vyaTB vimetulia, havitadhuru mtu na ***haviwezi kuenea kwa watu wengeni***. Mtu ameambukizwa lakini si mgonjwa na kuna uwezekano wa kutofahamu kwamba ameambukizwa.

## What is TB disease?

## Ugonjwa wa TB ni nini?

Kifua kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza ambao kwa kawaida unaathiri mapafu lakini unaweza kuathiri sehemu nyingine za mwili. Kinaenezwa kutoka kwa mtu hadi mtu mwingine kwa njia ya hewa kwa kupitia matone yaliyoambukizwa. Inawezekana kupata ugonjwa waTB mda mfupi baada ya vijidudu kuingia katika mwili, kama ulinzi wa mwili ni dhaifu. Ni rahisi pia kwa vidudu tulivu vya TB kuwa hai wakati ulinzi wa mwili unakuwa dhaifu. Hii inaweza kuwa miaka baadaye kutokana na kuzeeka , ugonjwa wa hatari, ugonjwa wa kisukari unaokuwa, utumizi mbaya wa madawa ya kulevya au pombe, au maambukizi ya VVU(Virusi Vya Ukimwi).



## What happens after the Mantoux skin test is read?

## Nini kinachotokea baada ya kipimo cha Mantoux kupitia ngozi kusomwa?

Kama kipimo ni hasi, hakuna kipimo cha ziada kinachohitajika kwa wakati huu, lakini unaweza kuhitaji kipimo kingine miezi michache baadaye, kufuatana na sababu ya kipimo.

Kama kipimo ni cha hakika, eksirei ya kifua na uchunguzi kimwili vitahitajika ili kuhakikisha hakuna dalili ya ugonjwa hai. Kama hakuna dalili za TB hai daktari atajadili uwezekano wa kutumia dawa ili kuzuia ugonjwa waTB kukua. Faida za kutumia dawa zinatokana na umri wa mtu, afya na msingi hatari wa ugonjwa wa TB.

## For further information contact the TB Clinic in your region:

## Kwa habari zaidi wasiliana na Kliniki ya TB katika eneo lako:

| | |
|---|---|
| Alice Springs | 8951 7548 |
| Darwin | 8922 8804 |
| Katherine | 8973 9049 |
| Nhulunbuy | 8987 0282 |
| Tennant Creek | 8962 4259 |

au

www.nt.gov.au/health/cdc

Centre for Disease Control

Northern Territory Department of Health

March 2012

## Further information

## Taarifa zaidi

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na** Kliniki ya TB katika eneo lako.

| | |
|---|---|
| Alice Springs | 89517548 |
| Darwin | 89228804 |
| Katherine | 89739049 |
| Nhulunbuy | 89870357 |
| Tennant Ck | 89624259 |

au www.nt.gov.au/health/cdc

Centre for Disease Control

Northern Territory Department of Health

May 2011

Translated by O.Ndayizeye, June 2012